darasahuru.ac.tz

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA**

**MTIHANI WA KUMALIZA MUHULA WA KWANZA**

**KISWAHILI KIDATO CHA TATU.**

**MUDA: SAA 3:00** **MEI 2025**

**MAELEKEZO**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na moja (11).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na chagua maswali mawili (02) kutoka sehemu C.
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu nay a kila swali.
4. Andika kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi.

**SEHEMU A (ALAMA 16)**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika jibu herufi ya jibu hilo katika kijitabu chako cha kujibia.

i. Ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja na kuendelea lakini hakuna muundo wa kiima na herufi.
A. Kiima B. Kiarifu C. Kirai D. Kishazi

ii. Ni mojawapo kati ya lugha ambazo husema kweli huhesabika kama lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika baadhi ya vipengele fulani kama vile lafudhi, msamiati na muundo.
A. Lugha mama B. Lahaja C. Msamiati maundo D. Lahaja za kijiografia

iii. Hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana nyingine iliyofichika. Yaani hadithi nzima ni kama sitiari.
A. Maghani B. Majigambo C. Istiara D. Mbazi

iv. Ni maneno ambayo yanayotoa taarifa zaidi kuhusu mtenda au mtendwa.
A. Nomino B. Kitenzi C. Kiwakilishi D. Kielezi

v. Neno ngeli katika lugha ya Kiswahili limetokana na lugha gani kati ya zifuatazo
A. Kihaya B. Kisukuma C. Kichaga D. Kinyakyusa

vi. Ipi ni njozi sahihi ya vipera vya semi?
A. Soga, nyimbo na nahau B. Mafumbo, Soga na maghani
C. Misemo, mafumbo na mizungu D. Methali , Mizungu na maghani

vii. Katika fasihi kuna vipengele vya umbo la ngazi katika kazi zake hivyo ukiwa mahiri katika vipengele hivyo vitaje kama vilivyoorodheshwa hapo chini
A. Ujumbe, mtazamo, dhamira, migogoro
B. Mandhari, msimamo, ujumbe, dhamira
C. Falsafa, miundo, ujumbe, wahusika
D. Lugha, migogoro, falsafa, mtindo

viii. Sehemu ya lugha inayoshughulikia maumbo mbalimbali ya maneno huitwa?
A. Sarufi mofolojia B. Sarufi sintaksia C. Sarufi fonolojia D. Sarufi semantiki

ix. Ipi kati ya zifuatazo si sifa ya fasihi simulizi?

darasahuru.ac.tz

A. Kuwa na hali ya utendaji
B. Kuonana fanani na hadhira ana kwa ana
C. Kutokupokea mabadiliko ya papo kwa papo
D. Kuwa kongwe zaidi.

x. Katika mfumo wa lugha silabi na silabi huunda
A. Neno B. Sentensi C. Herufi D. Aya

2. Oanisha maelezo yaliyopo katika orodha A na dhana zilizopo katika orodha B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. Neno pamoja na taarifa zote juu yake zilizomo ndani ya kamusi. | A. Utata<br>B. Rejesta |
| ii. Ni hali ya neno au senetensi kuwa na maana zaidi ya moja. | C. Simo<br>D. Mofimu |
| iii. Ni maneno yasiyo sanifu yanayoaanzishwa na kikundi cha watu Fulani wenye utamaduni mmoja. | E. Kitomeo<br>F. Kiimbo |
| iv. Ni neno linaloingizwa katika kamusi ili lifafanuliwe. | G. Kidahizo |
| v. Ni matumizi ya lugha kulingana na muktadha maalum. | H. Kiima |
| vi. Ni sehemu ya sentensi inayokaliwa na mtenda au mtendwa wa jambo. | I. Mkazo |

**SEHEMU B (ALAMA 54).**

3. a) Licha ya kuhudhuria vipindi vyote lakini bado Mwajuma anashindwa kuyaweka majina katika ngeli zake. Mkiwa katika makundi ya mjadala, mwelekeze Mwajuma ngeli za nomino zifuatazo kwa kuzingatia kigezo cha kisintiksia.
   i. Machungwa
   ii. Kipofu
   iii. Ugonjwa
   iv. Uzi

   b) Tumia nafasi hiyo ya mjadala pia kumsaidia Mwajuma kubaini maumbo ya O-rejeshi ya ngeli ambazo majina yafuatayo yanaweza kuingizwa.

   i. Tochi
   ii. Koti
   iii. Shule
   iv. Mbuzi

4. a) Eleza dhima moja ya mofimu iliyobebwa na mofu "ki" katika maneno yafuatayo.
   i. Kijiji
   ii. Kichovu
   iii. Akifika
   iv. Kijikaratasi
   v. Kiti hiki kimevunjika

   b) Toa mifano mubashara kwa kutofautisha mofimu tegemezi na mofimu huru.

darasahuru.ac.tz

5. Kipindi cha hivi karibuni tumekuwa tukishuhudia maneno mapya ya kiswahiliyakizungumzwa na baadhi ya Watanzania kama vile ugaigai, unyama mwingi,we! Kuweza,  we! Huogopi, ubaya ubwela n.k. Wewe kama mwanafunzi wa kidato cha tatu, eleza njia zinazotumika kuunda maneno hayo yanayozuka katika jamii.
6. Senteni huweza kuchnganuliwa kwa kuitumia mikabala tofauti tofauti. Kwa kujikita katika mikabala yote wa kimapokeo na kimuundo, changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya matawi (ngowe).
   i. Mtoto anacheza mpira polepole.
   ii. Mbuzi aliyenunuliwa jana ameuzwa leo.
7. Kiswahili ni kibantu. Thibitisha kwa kutumia vigezo vya kiisimu na kwa mfano.
8. a) Mzungumzaji yeyote wa lugha ni mfungwa huru, kwa kutumia mifano thibitisha mambo yanayochangia hali hiyo kwa hoja nne (04).
   b) Kwa kutumia mifano eleza miundo mitano (05) ya kiima.

**SEHEMU C (ALAMA 30)**

**Jibu maswali mawili (02) katika sehemu hii.**

9. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameleta njia mbalimbali za kihifadhi kazi za fasihi simulizi. Thibitisha dai hilo kwa hoja sita.
10. Baadhi ya wanafunzi wa kidato cha tatu hawaoni umuhimu wa kujifunza fasihi. Toa hoja sita kuwaelimisha wanafunzi hao kuhusu umuhimu wa somo hilo.
11. Hadithi ni mojawapo ya utunzi wa fasihi ambao una vipera vingi, kwa kutumia kipera cha kigano, tunga hadithi yenye kichwa cha habari kisemacho **"UMZANIAYE NDIYE KUMBE SIYE".**